TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)
(TAASISI YA HAKI ZA WASANII)
S.L.P 70624 Dar es salaam, Simu:+255785769223,+255767292581
Barua pepe:tarotanzania@gmail.com,Mitandao ya kijamiii:instagram/fb, taro.tz
Anwani ya Ofisi: Mtaa wa Kihonzile , Mkabala na Daraja la kuelekea Bagamoyo,
Kata ya Mabwepande , Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam

"Tunasimama kwa ajili ya Haki na Maslahi ya wasanii wote"

Ref.No: Taro /P/2022/ A06 **: Swahili Version:** Date: 28th February 2022

**MTAZAMO WA KISHERIA KUHUSU BASATA KUTOKUA NA UWAZI KATIKA KUSIMAMIA SHUGHULI ZA SANAA ZA KITAMADUNI ZINAZOFANYIKA NJE YA NCHI**

Rejea kichwa cha habari hapo juu. **Tanzania Artists Rights Organization (TARO)** au kwa lugha ya Kiswahili **"TAASISI YA HAKI ZA WASANII"** ni shirika lisilo la kiserikali lililosajiriwa na sheria ya Mashirika yasiyo ya kiserikali iitwayo **"Non Governmental Organization Act.No.24. of 2002"**, Mnamo tarehe **26/11/2021**. Lengo kuu la **TARO** ni kuiwezesha jamii ya kitanzania kushiriki kikamilifu katika kupambana na umasikini kwa kutumia sanaa na fasihi. Katika kuakikisha inafanikiwa kwenye lengo lake kuu tajwa, moja ya shughuli za TARO ni kusaidia kulinda haki na maslahi ya wasanii wote kuhusiana na kazi zao za sanaa.

Mnamo tarehe 27 Septemba 2021, Baraza la Sanaa Taifa (BASATA) walitoa taarifa kwa umma inayohusu "Mwaliko wa Kushiriki Sherehe za Maandalizi ya Kombe la Dunia 2022 KATARI (QUATAR)". Waliorodhesha wasanii wa fani mbalimbali walioalikwa na wakatoa siku 3 tu,kwa wasanii wa fani zilizoorodheshwa kufanya maombi BASATA kama watahitaji kushiriki. Ifahamike siku 3 ni ndogo sana kwa wasanii wote kupata taarifa na kushiriki, kwani kuna wasanii wengine walikua hawajasajiliwa BASATA. Ila BASATA hawakutoa muda wa kutosha kuwapa nafasi na wasanii hao kujisajili ili washiriki. Mpaka sasa hakuna taarifa yoyote kwa umma kuhusu mwaliko huo. BASATA hawajaeleza, ***wasanii gani wamechaguliwa?, utaratibu au vigezo gani vimetumika kuwachagua au vitatumika kuwachagua wasanii watakaoshiriki?.*** Kwasasa wasanii wachache waliofanya maombi ya kushiriki katika Mwaliko huo, wana wasiwasi kitakachotokea kwenye mualiko huu kitafanana na kilichotokea EXPO 2020 DUBAI.

Mnamo tarehe 21 Februari 2022, Baraza la Sanaa Taifa (BASATA) walianza kutoa taarifa za wasanii wa Tanzania kushiriki katika shughuli za sanaa na utamaduni katika maonyesho ya kimataifa ya **EXPO 2020 DUBAI**. Lakini hawakuwahi kuweka wazi kuhusu mchakato mzima wa wasanii wa Tanzania kushiriki katika maonesho hayo. Hii imeleta sintofahamu baina ya wasanii mbalimbali Tanzania na kuanza kuhoji. ***"Je ni utaratibu na vigezo gani vimetumika kuwachagua wasanii walioshiriki katika maonyesho ya EXPO 2020 DUBAI?."***

TARO tunaungana na wasanii kuhoji **uwazi** wa BASATA katika kusimamia shughuli za kitamaduni zinazohusiana na sanaa zinazofanyika nje ya nchi, kwasababu ya **vitendo mbalimbali vya kibaguzi** dhidi ya wasanii vinavyotekelezwa na BASATA.

**Narejea:** Mnamo tarehe 10 Septemba 2019, Msanii nguli wa Uchoraji, Bwana Lutengano Mwakisopile alishinda **Tuzo Ya Kimataifa Ya Ubunifu Ya Oscar (OSCAR OF AFRICAN CREATIVITY)** kwenye kipengele cha nakshi za rangi. Tuzo hizi zilitolewa Misri na waziri wa Vijana na Michezo (Prof Ashrab Sobhy). Bwana Lutengano alishindana na wasanii 60 kutoka nchi 20 za Afrika na kuwashinda wote. Lutengano ameipeperusha bendera ya nchi yetu vyema na kutangaza utamaduni wetu mbele ya Soko la kimataifa kwa njia ya sanaa ya uchoraji.Gazeti la **The Guardian** lilitangaza swala hili. Kitu cha kushangaza na kusikitisha sana, **BASATA** hawakuwahi kumtangaza wala kumpa heshima yake (Kuhenziwa), kwa kazi kubwa aliyoifanya. Lakini Mwezi mmoja mbele yaani 22 October 2019, **Diamond, Ray na Nandy** walishinda tuzo za **African Entertainment Award USA 2019,** lakini hawa walipewa heshima zao na kutangazwa (walihenziwa) na BASATA. Kitendo cha BASATA kutomtambua na kumuenzi **Lutengano Mwakisopile** kwa kazi kubwa aliyoifanya kinasanifu ubaguzi wa hali ya juu kwenye **sanaa ya uchoraji**.

Mnamo tarehe 22 Februari 2022, **Ubalozi wa India** nchini umetoa heshima kwa **Msanii Kili Paul** kwa kazi kubwa ya sanaa ya uchekeshaji kwa kuchanganya **tamaduni za kimasai na kihindi** kupitia nyimbo za kihindi. Pia mnamo tarehe 27 Februari 2022, **Waziri Mkuu wa India, Mheshimiwa Narendra Modi** kupitia mtandao wa Tweeter (wenye wafuasi milioni 76.3) ametambua sanaa ya **Kili Paul** na **Neema Paul** kwa ubunifu wa hali ya juu kupitia **tamaduni**. Lakini mpaka hivi leo, BASATA hawajawapa heshima yao wala kuwatangaza (Kuwaenzi) wasanii hao, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutangaza tamaduni za kitanzania kimataifa. Ni siku saba sasa zimepita tangu ubalozi wa India nchini utambue sanaa ya **Kili Paul** na **Neema Paul.**

## HOJA ZA KISHERIA

**Je ni wajibu wa BASATA kisheria kusimamia shughuli za sanaa zinazohusiana na utamaduni kwa uwazi?**

- **A.** Kwa mujibu wa kipengele cha **7.1.1**, Sura ya Saba ya **SERA YA UTAMADUNI (1999)** kinaelekeza kuwa *“ Kila mwananchi hana budi kutambua kuwa kushiriki katika shughuli mbalimbali za utamaduni wake ni haki ya msingi”*
- **B.** Kwa mujibu wa kipengele cha **7.1.4**, Sura ya Saba ya **SERA YA UTAMADUNI (1999)** kinaelekeza kuwa *“ itahikikishwa kwamba vyombo vilivyokabidhiwa dhamana ya kusimamia na kuendeleza fani mbalimbali za utamaduni vinaendesha shughuli zake kwa uwazi na kuzingatia sheria na demokrasia ili kuwapa fursa wananchi wengi kushiriki”*
- **C.** Kwa mujibu wa kipengele cha **9.4**, Sura ya Tisa ya **SERA YA UTAMADUNI (1999)** kinaeleza kuwa *“Serikali inatambua kwamba wajibu wa kuendeleza utamaduni siyo wake peke yake na hivyo ni lazima wananchi washirikishwe katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli hizi.”*



TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

D. Kwa mujibu wa kipengele cha **7.4**, Sura ya Saba ya **SERA YA MENEJIMENTI NA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA.Toleo 2, Septemba , 2008** kinaeleza kuwa *"Watumishi wa umma wanatakiwa kuielewa dira , malengo na maadili na wanawajibika kufuata utaratibu wa usimamizi uliowekwa kwenye sera hii. Kimsingi wanawajibu wa kuhudumia raia wote na wateja wengine kwa kiwango cha juu cha* ***uaminifu,*** *uadilifu na upole"*

E. Kwa mujibu wa kipengele cha **3(2)** cha **Kanuni za Maadili ya Utendaji wa Utumishi wa Umma 2005** kinaelekeza kuwa " *Kwa hiyo watumishi wa Umma wanatakiwa kutekeleza* ***sera*** *na maelekezo halali yanayotolewa na Mawaziri na viongozi wao wengine wa serikali"*

F. Kwa mujibu wa kipengele cha **4.5** cha **Ufafanuzi Kuhusu Maadili ya Utumishi wa Umma** 2006 kinaelekeza kuwa *" kufuata maelekezo ni kuzingatia* ***Sera****, Sheria, Kanuni na taratibu zinazotumika kwa watumishi wote"*

***Je ni takwa kisheria kuhimiza kutambuliwa kwa wasanii wenye uwezo na vipaji maalum vinavyohusiana na utamaduni?***

A. Kwa mujibu wa kipengele cha **9.4.2**, Sura ya Tisa ya **SERA YA UTAMADUNI (1999)** kinaelekeza kuwa *"wanachi watahimizwa kuwatambua watu wenye uwezo na vipaji maalumu vinavyohusu utamaduni miongoni mwao na kuwaenzi inavyopaswa"*

TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

## HITIMISHO

Kwa mujibu wa **SERA YA UTAMADUNI (1999)** ambayo BASATA kuitekeleza ni takwa kisheria, inaitaka BASATA kuwa na uwazi na ushirikishaji wa wananchi kwenye shughuli za sanaa zinazohusisha utamaduni. **SERA YA MENEJIMENTI NA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA** inawataka wafanyakazi wote wa BASATA kuwa na uaminifu wa hali ya juu. Hivyo basi taratibu za mazoea za BASATA kuwasiliana na viongozi wa vyama au mashirikisho ya sanaa fulani, bila kuwashirikisha wasanii/wananchi (taarifa kwa umma) katika shughuli za sanaa zinazohusiana na utamaduni sio kiwango cha uwazi, ushirikishaji wa wananchi na uaminifu wa hali ya juu unaohitajika na sera.

Kwa mujibu wa **SERA YA UTAMADUNI (1999)** wasanii wenye uwezo na vipaji maalumu vinavyohusu utamaduni wanahaki ya kutambuliwa na kuenziwa.

HIVYO BASI **TARO**, tunawataka BASATA kuwa na uwazi na ushirikishaji wa wananchi kwa uaminifu wa hali ya juu, kwa kujibu sintofahamu za wasanii kuhusu tamasha la **EXPO 2020 DUBAI** na **Mwaliko wa Kombe la dunia 2022 KATARI**. Pia **TARO** tunawataka BASATA kuwatambua na kuwaenzi **LUTENGANO MWAKISOPILE**, **KILI PAUL** na **NEEMA PAUL** kwa kazi nzuri za sanaa walizofanya kuhusiana na utamaduni za nchi yetu.

ASANTENI
MUNGU AIBARIKI TANZANIA
MUNGU ATUBARIKI WATANZANIA
(Kazi iendelee)

Wako katika kujenga Taifa

**Mkurugenzi Mkuu wa Utawala**
**WAKILI JOSHUA MSAMBILA**